**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA MAOMBI YA UFADHILI WA MASOMO YA UZAMILI KWA MWAKA 2022/2023

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya anawatangazia watumishi wote waliopata udahili wa kusoma masomo ya Shahada ya Uzamili (Masters Degree) katika fani za Afya kwa mwaka 2022/2023 kwamba, Wizara imeongeza muda wa kupokea maombi ya ufadhili kutoka tarehe **20/08/2022** mpaka tarehe **09/09/2022**. Muda huu umeongezwa ili kuwaruhusu watumishi ambao hawakuweza kuwasilisha maombi yao ndani ya muda uliowekwa awali kutokana na kutokuwa na barua za udahili kutoka kwenye vyuo walivyoomba kwenda kusoma.

Taratibu za kuwasilisha maombi ni zilizile ambapo maombi yatawasilishwa kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia ‘link‘ iliyotolewa kwenye tangazo hili. Maombi yatakayofanyiwa kazi ni yale yaliyowasilishwa kwa njia ya mfumo huu tu. Hivyo, waombaji waliowasilisha maombi yao kabla ya tangazo hili wanapaswa kufuata utaratibu huu.

Ufadhili huu ni kwa ajili ya kulipiwa ada ya mafunzo, posho ya kujikimu na nauli (wanafunzi watakaopata ufadhili nje ya nchi), pamoja na posho ya utafiti pindi mwanafunzi anapokuwa kwenye kipindi cha kufanya utafiti kama sehemu ya mafunzo yake. Malipo ya posho ya utafiti na posho ya kujikimu yatazingatia viwango vilivyopangwa na Wizara.

Vigezo vitakavyotumika kuwapata watakaofadhiliwa ni hivi vifuatavyo :

1. Kuwasilishwa kwa maombi rasmi ya ufadhili kwa njia ya mfumo (Post-graduate Sponsorship Online Application System)

2. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania.

3. Awe mtumishi wa Serikali

4. Awe ana barua ya udahili kutoka kwenye chuo kinachotambuliwa na Serikali ndani au nje ya nchi

5. Mwombaji awe amefanya kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu baada ya kuajiriwa Serikalini.

6. Ufadhili utazingatia uhitaji unaotokana na uhaba wa taaluma/fani kwenye kituo husika. Kwa mantiki hiyo, kipaumbele cha kupata ufadhili itategemea na upungufu wa taaluma aliyoomba kwenda kusoma kwenye kituo chake cha kazi.

7. Kipaumbele kitatolewa kwa:
    a. Kuzingatia mpango wa mafunzo wa kusomesha wataalam ulioandaliwa kwa ajili ya kutoa huduma maalum za kibobezi kwenye hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali maalum na Hospitali ya Taifa
    b. Watumishi wa Serikali ambao baada ya mafunzo watarudi kwenye vituo vyao vya awali au kupangiwa vituo vingine kulingana na uhitaji.
    c. Waombaji waliodahiliwa katika fani ambazo ni za kipaumbele katika utoaji wa huduma za kibingwa. Fani hizo ni *Anaesthesiology, Oncology, Psychiatry, Anatomical Pathology, Emergency Medicine, Surgery, Obstetrics and Gynaecology, Orthopaedics Surgery, Paediatrics, Internal Medicine, Dermatovenereology, Haematology,Radiology, Opthalmology, Otorhinolaryngology, Oral-Maxilofacial Surgery, Dentistry, Orthodentics,Infectious Disese Control, Microbiology and Immunology, Parasitology and Entomology, Critical/Intensive Care Nursing, Cardiovascular Nursing,Oncology Nursing, Nephrology Nursing, Cardiovascular perfusion in Nursing, Mental Health Nursing, Midwifery and Womens Health, Clinical Pharmacy, Pharmaconvigilance, Pharmaceutical Management, Epidemiology and Laboratory Management*
    d. Waombaji waliodahiliwa katika nyanja za Ubingwa Bobezi (Super-specialities) zenye umuhimu katika Hospitali Maalumu ili kujenga uwezo wa ndani ya nchi katika jitihada za kupunguza wagonjwa wa rufaa wanaotibiwa nje ya nchi pamoja na kuchochea tiba utalii katika Hospitali Maalum, Kanda na Taifa. Mfano wa taaluma hizo ni *Cardiology, Cardio-thoracic Surgery, Neonatology, Urology, Plastic & Reconstructive Surgery, Nephrology, Haematology, Pediatric Haemato-oncology, Paediatric Dentistry, Paediatric Oncology,*

*Forensic Medicine, Endocrinology, Paediatric anaesthesia, Obstetric Anaesthesia, Pulmunology, Gastroenterology, Interventional Radiography, Medical Imaging, Paediatric Neurology*

e. Waombaji waliodahiliwa kwenye taaluma za kimkakati ambazo mafunzo yake hayatolewi ndani ya nchi kwa mfano, *Vaccinology, Microbiology, Immunology, Angiology, Feto-maternal Medicine, Gyne-oncology, Pharmaceutical Industry, Medical Education, Geriatric Medicine, Theatre Management, Adolescent and paediatric psychiatric, Neurosurgery, Bone-marrow Transplant and Infectious Disease Control.*
f. Waombaji waliodahiliwa katika taaluma za afya za manejimenti na uendeshaji wa huduma za afya kwa mfano, *Health Monitoring and Evaluation, Health Systems Management, Health Policy and Planning, Health Economics, Health Financing, Health Promotion, Hospital management, Health Laws.*

8. Aidha, mwombaji atatakiwa awe ameambatisha nakala halisi ya nyaraka zifuatazo wakati wa kufanya maombi:
   a. Barua ya ruhusa ya masomo kutoka kwa mwajiri wake
   b. Barua ya udahili kutoka chuoni
   c. Cheti cha taaluma
   d. Cheti cha usajili na Leseni hai kutoka kwenye Baraza la taaluma husika
   e. Cheti cha kuzaliwa
   f. Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

Maombi yote yawasilishwe kwa kutumia ‘link’ ifuatayo:
***https://esponsorship.moh.go.tz/***

Kama ilivyoelekezwa hapo juu, mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 09/09/2022.

Imetolewa na:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Afya
Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya,
S.L.P 743
**40478 DODOMA**